

Public education  
Discover a world of opportunities

# KUSOMA: KUSOMEA NYUMBANI

## HATUA ZA KUSOMA

Mtoto wako hupitia hatua mbalimbali wakati wanajifunza kusoma. Kumbuka kwamba watoto hujifunza kwa njia tofauti na katika viwango tofauti, kwa hivyo kuwa na subira na daima hamasisha juhudi za watoto wako.

### Kusoma kwa mchezo wa kupokezana

Kama mtoto wako anavyokua na kuendelea, wanaanza kupenda vitabu na maneno wanavyo yaona karibu na wao.

Wanaweza kuanza kukuiga wewe kwa kushika vitabu kwa njia sahihi yaa juu, na kugeuza kurasa kwa makini na kujifanya kusoma kwa kutumia picha na kumbukumbu zao ili kusema hadithi. Pia wanafahamu fauti kati ya mbele na nyuma ya kitabu, huelewa maneno na picha ni tofauti, na kwamba maneno yaliyochapishwa yana ujumbe.

unaweza kuwasaidia watoto wako kwa:

- kusoma nawo kila siku
- kuhimiza na kusifia kwa kujaribu kwa kusoma
- kuwaonyesha kwamba picha zinasaidia kusema historia
- kusoma hadithi wanazozipenda mara kwa mara– kuzoea kunajenga kujiamini
- usiwapinge wanapofanya makosa – kujifunza kusoma kunachukua mda!

### Majaribio ya wasomaji.

Katika hatua hii, watoto wako mara nyingi husoma na kuangalia picha na kutumia kumbukumbu zao za hadithi. Pia hutambua baadhi ya maneno, lakini lengo lao linakuwa juu ya maana ya maandishi badala ya kusoma kila neno vizuri.

unaweza kuwasaidia watoto wako kwa:

- soma nao kila siku
- kuwahamasisha kujaribu kusoma kusoma na kuwasifukwa jitihada zao
- kuzungumza nawao kuhusu sauti, maneno na makala ya kuvutia katika vitabu na maandiko mengine kama maandiko, orodha ya ununuzi na magazeti
- kuzungumza nawao kuhusu wahusika kwenye kitabu na historia
- kuwatia moyo ili watoe maoni yao kuhusu nini kinatokea kwenye hadithi
- kuendelea kusoma hadithi zao wanazozipendelea mara kwa mara

**Zima televisheni. Ni rahisi mtoto wako kuweza kutulia kama hakuna vitu vya kumhangaisha.**



Department of  
Education

Utapata zaidi  
Kijitabu cha ukweli cha kusomea nyumbani  
Kwenye elimu hapa: [education.wa.edu.au](http://education.wa.edu.au).

# KUSOMA: KUSOMEA NYUMBANI

## Wasomaji wa wa mapema

Katika hatua hii, watoto wana uwezo wa kusoma maandiko wanayofahamu. Wakati wao husoma maandiko mpya, wanaweza kusoma polepole na kwa makusudi kuzingatia kila neno, ili kujaribu kusoma hasa vile ilivyoandikwa kwa ukurasa. Watoto wako wanaweza pia kuanza kukuambia vile wanafikiria kuhusu mambo waliyoyasoma na kwa nini wanafikiri hivyo.

unaweza kumsaidia mtoto wako kwa:

- kuwasomea mara nyingi na kuwatia moyo kuzungumzia juu ya hadithi
- kuwatia moyo watoe maoni kuhusu mambo wanayoyasoma
- kuonyesha na kuzungumza juu ya maneno ya kawaida

**Ni muhimu sana kuwapatia watoto wako kura ya sifa wakati anajifunza kusoma. Epuka kuwapinga kama wakikosea, hata kama ni rahisi kwako. Baadhi ya watoto wanahitaji mazoezi mengi na kutiwa moyo.**

- kuwahamasisha kujaribu njia tofauti katika kutafuta kujua maneno wasiyoyafahamu kama vile kutaja neno kwa sauti, kwa kutumia picha za maonyesho na dalili zingine unazowapa, kusoma sentensi tena, na kusoma hadi mwishoni mwa sentensi
- kuwauliza kuhusu nini wanafikiria juu ya kilichotendeka katika hadithi, na kwa nini wanafikiri mhusika alisema au alifanya kitu fulani
- kuwahamasisha kusema kuhusu jinsi ya kutafuta kujua neno ambalo hawalijui
- kuandika maelezo juu ya ujumbe wa bodi kwa ajili yao kuweza kusoma na kuwahamasisha kuandika maelezo pia

